— Jipya —

# TANGAZO LA KAZI ZA UJENZI

Tarehe: 09/03/2019

## TANGAZO LA ZABUNI KWA AJILI YA MAFUNDI WA UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA KATIKA SHULE YA SEKONDARI WELA

Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imepokea fedha toka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa kuanzia msingi mpaka kupauwa katika shule ya sekondari wela kwa mwaka wa fedha 2018-2019

Kamati ya ujenzi ya shule ya sekondari Wela inawatangazia Mafundi wote wa ujenzi wenye uwezo wa kujenga vyumba viwili vya madarasa kuomba kazi ya kujenga vyumba hivyo. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega katika shule ya sekondari Wela.

Ujenzi wa vyumba hivyo utafanyika kwa utaratibu wa kutumia "Force Account".

**Sifa za mwombaji:-**

a. Muombaji awe na uzoefu wa kujenga majengo yanayofanana na kazi anayoomba (majengo ya serikali yatakuwa na faida zaidi) mwenye uangalizi mzuri wa mali wakati wa utekelezaji wa mradi huo.
b. Muombaji ajue vyema kusoma ramani na vipimo vyake kwa ajili ya ufanisi wa kazi
c. Muomba[illegible] mchanganuo wa muda wa utekelezaji mradi.
d. Maombi y[illegible] kuwa hai kwa muda wa siku **45** baada ya kufunguliwa.
e. Muombaji awe na akaunti benki itakayowezesha malipo kwa njia ya hundi

JIPYA

f. Kuwa na cheti cha ufundi ni sifa ya ziada.
g. Muombaji awe na barua ya utambulisho wa eneo analotoka
h. Muombaji awe na barua ya mdhamini kwa kazi husika
i. Waombaji/Mafundi watatakiwa kuonesha kazi ambazo wamewahi kuzifanya pamoja na namba za simu za wateja wao waliowafanyia kazi hizo katika kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita.

Aidha kila mwombaji atatakiwa kuonyesha gharama za ufundi za ujenzi huo. Mchoro wa majengo hayo pamoja na mchanganuo wa kazi zitakazofanyika vinapatikana kwenye ofisi ya Mkuu wa Shule sekondari ya Wela kwa ajili ya rejea kabla ya kujaza bei.

Mafundi watachaguliwa kwa kuzingatia sifa walizoambatanisha, gharama za ufundi pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za Ununuzi wa Umma.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **18 Machi, 2019 saa saba kamili mchana na waombaji wote wanatakiwa wawepo.** Maombi yatakayochelewa baada ya muda tajwa hapo juu hayatapokelewa kwa ajili ya tathmini. Ufunguzi wa zabuni utafanyika mara baada ya muda wa kupokea zabuni kuisha.

Maombi yote yatumwe katika Ofisi ya Mkuu wa Shule, Shule ya Sekondari Wela kwa anuani ifuatayo:-

MKUU WA SHULE,
SEKONDARI YA WELA,
S. L. P 316,
**NZEGA.**

**Gharama za maombi hayo ni shilingi 20,000.00 (elfu ishirini tu) ambazo hazitarudishwa**

**Imeandaliwa na;**

……………………….

**TEOPISTA KACHINDE**

HEADMISTRESS
WELA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 316-NZEGA